



TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEO	MAELEZO/ ENEO	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Hosteli za Ubungo	Eneo lina uwezo wa kuhudumia takribani watu 180	Mgahawa mdogo wa chakula
2.	Hosteli za Ubungo	Chumba kilichopo ndani ya Kantini	Steshenari
3.	Kampasi ya Kijitonyama	Chumba Namba 2	Steshenari
4.	DARUSO Bar	Kampasi ya Mwl. Julius Nyerere, Mlimani. Katika eneo hili hairuhusiwi kuuza vyakula vinavyopikwa katika Kafeteria za jirani	Vinywaji laini na vikali

Kwa tangazo hili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma. Waombaji wafike Ofisi ya Chuo ya Uwekezaji chumba Namba 228 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi elfu kumi tu (TZS 10,000/=) kupitia 'Namba ya Kumbukumbu' ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili. Tarehe **5 Januari 2023** itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi tutakutana katika eneo la Kampasi ya Hosteli za Ubungo na Saa 6:00 Mchana tutakutana katika eneo la CoICT Kampasi ya Kijitonyama na kuanzia saa 8:00 mchana tutakutana katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo hayo kwa njia ya barua.

Imetolewa na
NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA
27.12.2022